

# NYSITELL kitabu kidogo cha Taarifa kwa Mzazi

Swahili | August 2015

**Karibuni katika mfumo wa shule za Jimbo la New York! ujumbe ya Idara ya Elimu ya Jimbo la New York (NYSED) Ofisi ya Elimu ya Lugha Mbili na Lugha za Dunia (OBEWL) ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wa Jimbo la New York (NYS), ikiwa ni pamoja na Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELLs) / Wanafunzi wa Lugha Nyingi (MLLs), wanafikia cheo cha juu cha mafanikio ya kitaaluma na ustadi wa lugha. Tunajitahidi kuhakikisha kuwa wanafunzi wote'njia moja ya elimu na mahitaji ya hisia za kijamii zinafikiwa katika lugha nyingi zitakazowapelekea katika utayari wa chuo kikubwa na katika kufanya kazi.**

## UTANGULIZI

Katika uandikishaji ulionyesha kuwa lugha ya msingi ya mtoto wako nyumbani ni ingine isiyokuwa Kiingereza, na mkufunzi alimuhoji ili kuamua kama inawezekana haja ya msaada wa ziada kwa lugha ya Kiingereza. Taarifa zilizokusanywa wakati wa mahojiano zilionyesha kuwa mtoto wako anaweza kuwezeshwa kwa huduma za ELL na kutambulika kama ELL / MLL. Ili kuthibitisha uhakika wa mtoto wako kwa msaada wa ziada wa lugha ya Kiingereza, mtoto wako sasa atapatiwa Jaribio la Kutambuliwa la Jimbo la New York kwa Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (NYSITELL).

## NINI MADHUMUNI YA NYSITELL?

Madhumuni ya NYSITELL ni kutathmini kiwango cha lugha ya Kiingereza cha wanafunzi wapya ambao lugha ya msingi nyumbani ni ingine isiyokuwa Kiingereza. Alama atakazopata mtoto wako katika NYSITELL (Wakati wa Kuingia, Kuchipukia, Kipindi cha mpito, Kupanuka, au Kuongoza) zitaamua kama yeye ana haki ya kupata huduma ya ELL na kuamua kiwango cha msaada wa lugha ya Kiingereza. Matokeo pia yatawasaidia walimu kupanga mpango bora kwa mtoto wako kulingana na uwezo wake na mahitaji katika kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika katika lugha ya Kiingereza.

## WAKATI GANI (NYSITELL) ITATOLEWA?

NYSITELL itaamuriwa iwezekanavyo ELLs/MLLs mara moja kufuatia kuandikisha katika mfumo wa shule wa Jimbo la New York.

## NI MASWALI YA AINA GANI WANAFUNZI WATAULIZWA?

NYSITELL ni pamoja na uchaguzi mingi, majibu ya maswali ya kuchagua, kujibu maswali mafupi ya kuandika, kujibu maswali marefu ya kuandika, na kujibu maswali kwa mdomo katika kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika.

## VIPI NITAPATA MATOKEO?

Shule ambayo mtoto wako ameandikishwa itamtumia mzazi barua ya taarifa ambayo iaotnyesha kiwango na hatua zozote za ziada ambazo unahitaji kuchukua. Kama mtoto wako atatambuliwa kama ELL / MLL, utatakiwa kuhudhuria kikao cha maelekezo wakati ambao utajifunza kuhusu programu za ELL ambazo zitakuwepo kwa ajili ya mtoto wako.

## VIWANGO VYA USTADI VINAMAANISHA NINI?

Kwa kutegemea alama ambazo mtoto wako atapata, anaweza kuzingatiwa kama yeye ni ELL/MLL. Maelezo ya viwango vya ustadi yametolewa hapa chini:

| Kiwango | Maelezo ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza | |
|---|---|---|
| Kuingia (Kiwango cha Kuanzia) | Mwanafunzi katika kiwango cha Kuingia ana utegemezi mkubwa katika misaada na miundo ya kuendelea katika stadi za lugha kitaaluma na bado hajafikia kiwango kinachohitaji katika kuonesha ustadi wa lugha ya Kiingereza katika mazingira kadhaa ya kitaaluma. | Wanaostahili Kupata Huduma |
| Kuchipukia (Kiwango cha Kati, Chini) | Mwanafunzi katika kiwango cha Kuchipukia ana utegemezi fulani katika misaada na miundo ya kuendelea katika stadi za lugha kitaaluma na bado hajafikia kiwango kinachohitajika katika kuonesha ustadi wa lugha ya Kiingereza katika mazingira kadhaa ya kitaaluma. | |
| Kipindi cha Mpito (Kiwango cha Kati) | Mwanafunzi katika kiwango cha Mpito anaonyesha utegemezi fulani katika kuendelea na stadi za lugha kitaaluma, lakini bado hajafikia mahitaji ya kilugha yanayohitajika katika ustadi wa lugha ya Kiingereza katika mazingira kadhaa ya kitaaluma. | |
| Kupanuka (Kiwango cha Juu) | Mwanafunzi katika kiwango cha Kupanuka anaonyesha uhuru mkubwa katika kuendeleza stadi za lugha kitaaluma na anakaribia mahitaji ya kiisimu yaohitajika ili kuonyesha ustadi katika lugha ya Kiingereza katika mazingira kadhaa ya kitaaluma. | |

## NANI WANAOANDAA NA KUFANYA MAJARIBIO

Majaribio huandaliwa na NYSITELL na hufanywa na waelimishaji waliohitimu wa Jimbo la New York.

## IKIWA MTOTO WANGU ANA IEP, MAJARIIBIO YA MAKAZI YANARUHUSIWA WAKATI WA NYSITELL?

Ndio, majaribio ya makazi kwa wanafunzi walio katika program ya IEP yanaruhusiwa katika NYSITELL. Zungumza na mwalimu wa mtoto wako ili kupata taarifa mahususi kuhusu makaazi ambayo mtoto wako anastahili.

## HUDUMA GANI AMBAZO MTOTO WANGU ANASTAHILI MARA TU ANAPOTAMBULIWA KAMA NI ELL/MLL?

Mara mtoto wako kutambuliwa kama ni ELL / MLL, atakuwa na haki ya: Elimu ya Lugha Mbili (katika Kiwango cha (Mpito au Lugha Mbili) na / au huduma za Kiingereza kama Lugha Mpya (ENL). Kiwango cha Ustadi cha mtoto wako huamua dakika katika huduma za ELL (muda wa darasa) atakaopatiwa kila wiki. Angalia chati ya chini kwa muda wa dakika maalum kulingana na kiwango cha ustadi.

| Kiwango | Daraja ya K-8 Dakika za Kusomeshwa ENL kwa Wiki | Daraja ya 9-12 Dakika za Kusomeshwa ENL kwa Wiki | Wanafunzi katika Programu za Lugha Mbili |
|---|---|---|---|
| Kuingia (Kiwango cha Kuanzia) | Dakika 360 | Dakika 540 | • Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani<br>• Kiwango cha chini cha maudhui ya masomo 2 katika lugha mbili |
| Kuchipukia (Kiwango cha Kati, Chini) | Dakika 360 | Dakika 360 | • Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani<br>• Kiwango cha chini cha maudhui ya masomo 2 katika lugha mbili |
| Kipindi cha Mpito (Kiwango cha Kati) | Dakika 180 | Dakika 180 | • Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani<br>• Kiwango cha chini cha maudhui ya somo 1 katika lugha mbili |
| Kupanuka (Kiwango cha Juu) | Dakika 80 | Dakika 180 | • Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani<br>• Kiwango cha chini cha maudhui ya somo 1 katika lugha mbili |

## MARA NIPATAPO MATOKEO, VIPI NINAWEZA KUSAIDIA NYUMBANI?

- Msomee mtoto wako katika lugha yake ya msingi au ya nyumbani na / au katika lugha ya Kiingereza (utafiti unaonyesha kuwa kumsomea mtoto wako katika lugha yake ya nyumbani itamsaidia katika ujuzi wa kusoma na kuandika Kiingereza).
- Mtolee hadithi mtoto wako katika lugha yake ya msingi au ya nyumbani.
- Tembelea maktaba ya eneo lako na azima vitabu vya kielektroniki vya kusikiliza vilivyo katika lugha yake ya msingi au ya nyumbani au Kiingereza.
- Hakikisha unahudhuria mikutano ya walimu na wazazi inayopangwa na shule ya mtoto wako.
- Panga mkutano binafsi na mwalimu wa mtoto wako ili kujifunza njia maalumu ambazo unaweza kumsaidia mtoto wako kufanikiwa.
- Panga wakati kila siku kwa mtoto wako wa kufanya kazi za nyumbani na ikiwezekana, mtafutie pahali penye utulivu, pasipo na usumbufu, ambapo anaweza kufanya kazi.
- Andaa matembezi ya kifamilia katika makumbusho. Miongozo katika makumbusho yanaweza kukusaidia kutembelea maonyesho pamoja na mtoto wako.
- Makumbusho na maktaba mara nyingi hutoa ofa za gharama nafuu/au bure wakati wa baada ya shule au wikiendi.

Kwa ajili ya maswali au mashaka kuhusu huduma za ELL tafadhali wasiliana na:
nysparenthotline@nyu.edu
Nambari ya Simu ya ELL kwa Mzazi: (800) 469-8224

**maswali Zingine?**
Tafadhali tuma maswali au maoni yako kwa Ofisi ya Elimu kwa Lugha Mbili na Lugha za Dunia OBEFLS@nysed.gov

Kwa maelezo zaidi juu ya NYSITELL tembelea tovuti hii:
http://www.p12.nysed.gov/assessment/nysitell/

NYSED.gov